

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**22 JUNI, 2023**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA HAMSINI NA TATU – TAREHE 22 JUNI, 2023

#### I. DUA:

#### II. MASWALI:

##### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

##### 694. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaipandisha hadhi barabara ya Mjele – Ikuwa hadi Mlima Njiwa kuwa ya Mkoa.

##### 695. MHESHIMIWA ALLY YAHYA MHATA (NANYUMBU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itafanya ukarabati katika Kituo cha Afya cha Nanyumbu.

**696. MHESHIMIWA JONAS WILLIAM MBUNDA  
(MBINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga kwa kiwango cha changarawe Barabara ya Mbanga, Kikolo hadi Kihungu ili iweze kupidika wakati wote.

**697. MHESHIMIWA SHABAN OMARI SHEKILINDI  
(LUSHOTO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka Gari la Wagonjwa katika Kituo cha Afya cha Mlola Wilayani Lushoto.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**698. MHESHIMIWA ENG. STELLA MARTIN  
MANYANYA (NYASA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvubi:-

Je, lini Soko la Samaki Mbamba Bay litaanza kutumika.

## **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

### **699. MHESHIMIWA JOSEPH MICHAEL MKUNDI (UKEREWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini kipande cha Barabara cha Kisorya hadi Nansio kitaanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

## **WIZARA YA KILIMO:**

### **700. MHESHIMIWA JESCA JONATHANI MSAMBATAVANGU (IRINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali imejipangaje kutatua chagamoto ya upatikanaji wa mbolea nchini.

### **701. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (BLW):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kwa kiwango gani TEHAMA inatumika kuboresha Sekta ya Kilimo nchini.

## **WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

### **702. MHESHIMIWA SUBIRA KHAMIS MGALU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, upi mpango wa kuwapa mafunzo Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi ngazi za Vitongoji, Vijiji, Kata na Wilaya - Pwani.

### **703. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapatia msaada wa Kisaikolojia Watu waliopitia ukatili wa kijinsia.

### **III. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge sasa likubali Kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA**  
**22 JUNI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***  
**KATIBU WA BUNGE**